

TAARIFA YA MRADI WA KIWANDA CHA KUFYATUA TOFALI UNAOOTEKELEZWA NA PINAKA LOGISTICS LTD MBINGA MJINI KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAFI NDUGU, CHARLES FRANCIS KABEHO TAREHE 05.06.2018

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018 , Ninayo furaha kubwa kukukaribisha pamoja na Msafara wako wote.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Mradi wa kufyatua tofali za Saruji (vibrated blocks) ulianzishwa mwezi Februari 2017 kwa machine moja ndogo yenye thamani ya shilingi million 40 yenye uwezo wa kufyatua tofari 1500 kwa siku, ila kwa sasa nimeweza kuongeza machine nyingine ya pili kubwa yenye thamani ya million 120 yenye uwezo wa kufyatua tofari 3000 kwa siku na jumla ya machine zote mbili zina thamani ya million 160. Machine zote mbili zinatumiwa mfumo wa Maji, Vibao, Fensi, Machine Kuu, Mixer na Froma kwa undeshaji.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Huduma za tofali tunazozalisha kwenye kiwanda chetu ni za inchi 6, inchi 5, inchi 4 and Pavement Blocks, Pia kiwanda chetu kinatengeneza tofali za kiwango cha kiserikali kwa viwango vya Bs kwa oda.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Uwepo wa kiwanda chetu hapa Mbinga mjini kimezalisha ajira za kudumu 30 na ajira sisizo za kudumu (vibarua) 100 na zinawasaidia kusomesha watoto wao na kumudu maisha yao kwa ujumla, vile vile tumeweza kutoa elimu kwa wafanyakazi 30 jinsi ya kuendesha mitambo hiyo kwani **“Elimu ni Ufunguo wa Maisha; Wekeza sasa kwa Maendeleo ya Taifa letu”**

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Malengo kwa sasa ni kuongeza uzalishaji wa tofali kwa wingi na kuwaelimisha Wananchi kutumia tofali za kisasa (vibrated blocks) kwani hutunza mazingira tofauti na matumizi ya tofali za udongo zinazoharibu mazingira.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Baada ya taarifa hii, kwa heshima na taadhima naomba uzindue kiwanda changu.

Ni mimi

**VALLENCE URIO.
MKURUGENZI.
PINAKA LOGISTICS LTD**